TALKING NOTES ZA MHE. THOBIAS E. M. ANDENGENYE, MKUU WA MKOA WA KIGOMA WAKATI AKIZUNGUMZA NA WAJUMBE WA BARAZA LA MADIWANI LA HALMASHAURI YA WILAYA BUHIGWE
TAREHE 04 JUNI, 2021

UTANGULIZI

Mhe. Venance Sylvester Kigwinya - Mwenyekiti wa Halmashauri,

Mhe. Col. Michael Masala Ngayalina - Mkuu wa Wilaya,

Mhe. Eles Elia Gomwa - Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri,

Ndg. Marycelina Coelestine Mbehoma - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W),

Ndg. Vallence Rutakyamirwa - Mkaguzi Mkuu wa Nje (NAOT),

Ndg. Barongereje Gerald Nkabe - Mwenyekiti wa CCM (W),

Ndg. Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Ndg. Wajumbe wa Kamati ya Usalama ya Wilaya,

Wah. Madiwani,

Ndg. Watendaji katika ngazi mbalimbali,

Ndg. Wageni Waalikwa,

Ndg. Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri,

- Natoa Shukrani kwa Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya Buhigwe kwa Mwaliko wa kushiriki na kuzungumza na Wajumbe wa Baraza la Madiwani na Wananchi waliofika kufuatilia Mkutano huu Maalum wa kujadili **Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020**.

- Huu ni Mkutano wangu wa kwanza kuhudhuria katika Halmashauri yenu tangu nilipoteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma.

- Mwaliko niliopewa ni jambo la heshima kwangu na litanipa fursa ya kusikiliza namna mnavyoendesha majadiliano yenu na kuwashauri kadri itakavyohitajika.

- Nawapongeza kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yenu licha ya changamoto kadhaa mnazokabiliana nazo.

- Nawashukuru nyote kwa mahudhurio yenu mazuri.

TAARIFA YA CAG KWA HESABU ZA MWAKA 2019/2020

Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri,

- Nimesoma Ripoti Kuu ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo pamoja na mambo mengine imeonesha kuwa Halmashauri yenu ni miongoni mwa

Halmashauri 53 Nchini zilizopata Hati yenye Shaka.

- Kama mnavyofahamu, Halmashauri yenu imepata Hati yenye Shaka kwa mwaka wa pili mfululizo baada ya kupata Hati inayoridhisha (Hati Safi) kwa miaka mitano (5) mfululizo tangu Halmashauri yenu ilipoanzishwa rasmi katika mwaka wa fedha 2013/2014.

- Halmashauri nyingine zilizopata Hati zenye Shaka kwa Mkoa wa Kigoma ni; Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji, Halmashauri ya Mji Kasulu, Halmashauri ya Wilaya Kakonko, Halmashauri ya Wilaya Kasulu na Halmashauri ya Wilaya Uvinza. **Hali hii imeutia doa Mkoa wetu.**

- Pamoja na kupata Hati yenye Shaka, Halmashauri yenu pia ni miongoni mwa Halmashauri 93 nchini zilizopata **Aya ya Masuala ya Mkazo** *(Emphasis of Matters)*. Aya hiyo kwa Halmashauri hii inahusu;

  Kesi dhidi ya Halmashauri zenye thamani ya sh. 17,440,000 ambazo zinaweza kuiathiri Halmashauri kifedha iwapo zitaamuliwa kwa kuwapa faida wadai/walalamikaji. Nashauri Halmashauri ifikirie namna ya kuyamaliza mashauri hayo nje ya Mahakama.

- Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebainisha msingi wa Halmashauri yenu kupata Hati yenye Shaka kuwa ni;

  a. Tofauti isiyo na maelezo kutokana na kiasi kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha zilizokaguliwa mwaka jana (2018/2019)

na kiasi cha ulinganisho kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha kwa mwaka huu (2019/2020) ya Sh. 1,981,864,000

Maelezo Na. 14A kwenye taarifa za fedha yalionesha matumizi yaliyotokana na mishahara na stahiki za watumishi kwa mwaka wa ulinganisho (2019/2020) ya Sh. 12,491,002,000; lakini kiasi cha mishahara na stahiki za watumishi kilichooneshwa kwenye taarifa za (2018/2019) kilikuwa Sh.14,472,866,000, hivyo kupelekea tofauti ambayo haikutolewa maelezo ya Sh. 1,981,864,000.

b. Marekebisho yaliyotokana na madeni ya stahiki za watumishi hayakuoneshwa sawasawa kwenye taarifa za fedha, Sh. 542,711,000

Maelezo Na. 42 na 28 kwenye taarifa za fedha yalionesha masahihisho ya makosa yaliyofanyika ya mishahara na stahiki za watumishi kutoka Sh. 2,049,559,000 kilichooneshwa kwenye taarifa za fedha kufikia tarehe 30 Juni 2019 hadi Sh. 1,506,848,000 kilichooneshwa kama kiasi cha ulinganisho kwa kupunguza madeni ya Sh. 542,711,000, lakini hakukuwa na muamala ulioonesha eneo lililoongezeka (*credit entry*) kulingana na kupungua kwa madeni hayo. Pia, maelezo juu ya chimbuko la makosa hayo ya mwaka 2018/2019 halikuelezewa, hivyo Mkaguzi ameshindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wake.

- Ninawashauri mfanye marekebisho yanayotakiwa ili hoja hizo zifungwe kabla ya ukaguzi ujao. Aidha, hakikisheni mnawasilisha Kitabu chenu pamoja na marekebisho yake (iwapo yatafanyika) kwa wakati ili muweze kuepukana na hoja za aina hiyo wakati mwingine**.**

- Pamoja na hoja hizo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebainisha mapungufu mengine kwenye hesabu zenu kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Baadhi ya mapungufu hayo ni;

  - Manunuzi yaliyoambatishwa stakabadhi za kielekitroniki zenye kutia shaka sh. 34,720,000. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaamini kuwa Miamala hii imefanyika kutokana na udhaifu katika udhibiti wa ndani wa halmashauri na halmashauri yenu kushindwa kufanya tathmini ya vihatarishi vya udanganyifu ili kubaini na kuzuia kutokea kwake. *Naelekeza, uchunguzi wa kina ufanyike ili kubainisha kiasi halisi cha upotevu wa fedha za umma na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika.*

    Aidha, Menejimenti ya Halmashauri inapaswa kuimarisha udhibiti wa ndani na kufanya tathmini ya vihatarishi vya udanganyifu kila wakati ili kubaini na kuzuia udanganyifu kabla haujatokea.

  - Halmashauri ilikuwa na Watumishi **41** wanaopata mishahara chini ya theluthi moja. Hali hii inaweza kuathiri utendaji wa watumishi husika na kuathiri utendaji wa jumla wa Halmashauri. *Nawakumbusha*

Maafisa Masuuli kwamba hawapaswi kuidhinisha mikopo ya Watumishi inayozidi kiasi kilichoidhinishwa.

- Malipo yenye thamani ya sh. 37,375,000 yalifanyika bila kuwa na Risiti za Kielektroniki (EFD). *Naelekeza wazabuni husika wafuatiliwe ili waweze kutoa risiti hizo na ziwasilishwe kwa Mkaguzi kwa uhakiki*.

- Madai ya muda mrefu na malipo yaliyofanywa na Halmashauri kabla ya kupokea huduma (sh. 24,787,000). *Nashauri muongeze nguvu katika kukusanya ili shughuli zilizopangwa ziweze kutekelezwa.*

- Halmashauri ilinunua vifaa vyenye thamani ya Sh. 143,490,849 zaidi ya Mahitaji. Hali hiyo ilisababishwa na makadirio yasiyo sahihi au kuzidisha kwa makusudi vifaa vinavyohitajika. kuna wasiwasi kwamba, kutokana na ukosefu wa vifaa vya kuhifadhia kuna uwezekano wa kupoteza vitu vilivyonunuliwa kupitia wizi au kuharibika. *Ninaelekeza kwamba takwimu za mahitaji ya vifaa kwa kazi za ujenzi zinapaswa kuandaliwa vizuri ili kuepuka manunuzi ya vifaa vingi kuliko mahitaji.*

- Halmashauri haikupeleka asilimia Ishirini ya fidia ya vyanzo vilivyofutwa kwenda kwenye Vijiji (sh. 178,004,179). *Taarifa inaonesha kwamba Halmashauri yenu haina utaratibu wa kupeleka fedha hizo katika ngazi za Kata na Vijiji. Nawashauri mpeleke fedha hizo ili zikachochee maendeleo na Utawala bora katika ngazi za Kata na Vijiji.*

- Halmashauri yenu haijachangia sh. 19,359,290 ambayo ni asilimia 10 ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Wenye ulemavu. *Tengeni fedha hizo na kulipa madeni yote.*

- Miamala iliyofutwa bila kuwepo kwa viambatisho muhimu (Sh. 13,681,473). Hali hii inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma. *Naelekeza kwamba mhakikishe marekebisho yote ya miamala yanakuwa na viambatisho muhimu na ili kuzuia matumizi mabaya ya fedha zinazokusanywa.*

- Mapato yaliyokusanywa na wakusanya mapato bila kupelekwa benki (sh. 57,156,802). *Nawashauri muimarishe usimamizi wa mikataba kati ya Halmashauri na wakusanya mapato na muwafuatilie waliokusanya fedha hizo ili zipatikane na ziweze kupelekwa benki.*

Taarifa kamili ya hoja zote za mwaka 2019/2020 na hoja za miaka ya nyuma (ambazo hazijafungwa) itawasilishwa na kujadiliwa katika Mkutano huu.

- Hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma inaonesha kwamba mapendekezo **35** yalitolewa kwa Halmashauri yenu ambapo mapendekezo **4** yametekelezwa, mapendekezo **8** yako katika hatua ya utekelezaji, mapendekezo **11** yamejirudia, pendekezo **1** limepitwa na wakati na mapendekezo **11** hayajatekelezwa. **Hali ya utekelezaji hairidhishi.**

Nashauri mjiwekee mkakati madhubuti wa kutekeleza mapendekezo yote ya miaka ya nyuma yaliyosalia.

MAELEKEZO YA NYONGEZA KUHUSU TAARIFA YA CAG

Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri,

- Katika mkutano wa leo mnalo jukumu la kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria Watumishi waliobainika kuhusika na vitendo vya ubadhirifu na kutowajibika ipasavyo na hivyo kuiletea Halmashauri yenu hasara na hoja ambazo katika hali ya kawaida ya utendaji makini zisingepaswa kutokea. Uchukuaji huu wa hatua ulenge Watumishi wote waliohusika katika ngazi zote (ngazi za chini, kati na Makao Makuu ya Halmashauri).

- Hakikisheni mnaimarisha uwajibikaji kwenye usimamizi wa fedha na rasilimali nyingine, zingatieni taratibu za fedha na imarisheni mifumo ya udhibiti wa ndani.

- Hakikisheni hoja za miaka ya nyuma haziendelei kujirudia. Mtafanikisha hilo kwa kuzingatia maoni/ushauri wa Mkaguzi na kufuata taratibu za fedha/malipo kwa usahihi. *Ni vyema pia mkawachukulia hatua wanaosababisha hoja kujirudia.*

- Hakikisheni hoja za ukaguzi zinajibiwa mapema na majibu kuwasilishwa kwa Mkaguzi Mkuu wa Nje ili afanye uhakiki.

- Wekeni mikakati na mipango madhubuti kuhusiana na mapungufu yote yaliyojitokeza ili kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo yote ya ukaguzi unafanikiwa. Mikakati hiyo inatakiwa iwe na uhalisia kiutekelezaji; itekelezwe kwa muda uliopangwa na iweke bayana namna ya utekelezaji.

- Halmashauri itenge Bajeti ya kutosha ili kuweza kuwapeleka Wahasibu na Wakaguzi kwenye Mafunzo ya mara kwa mara yanayoendeshwa na wataalamu wa Ufungaji wa Hesabu ili kuweza kupata miongozo mipya na marekebisho yake (IPSAS).

- Halmashauri itoe kipaumbele katika maandalizi ya Hesabu za Mwisho kwa kuhakikisha waandaaji wanawekewa mazingira mazuri wakati wa zoezi hilo na kuwaondolea mwingiliano kati ya jukumu hilo na majukumu yao mengine ya kila siku.

- Menejimenti ya Halmashauri ihakikishe Taarifa ya Fedha inaandaliwa kwa usahihi na kuzingatia miongozo na viwango vinavyoelekezwa.

- Afisa Masuuli ahakikishe unakuwepo uhusiano mzuri/ushirikiano kati ya Menejimenti za Halmashauri na Wakaguzi wa Nje na wahakikishe nyaraka zote zinazohitajika zinapatikana kwa wakati.

MASUALA YA KUZINGATIA

Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri,

Masuala yafuatayo yazingatiwe:

i. Zingatieni Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utekelezaji wa Majukumu yenu. Katika eneo hili mnaongozwa na Kanuni za Maadili ya Madiwani na Kanuni za Maadili kwa Watumishi wa Umma. Ni utovu wa Maadili na ni uvunjaji wa Sheria kwa Wah. Madiwani na Watumishi wa Umma kutumia nafasi na Madaraka yao kujipatia Mikataba na Zabuni mbalimbali ni makosa pia kwa Viongozi na Watendaji kutumia vibaya fedha na mali nyingine za Serikali.

ii. Simamieni ubora na viwango katika Miradi inayotekelezwa kwenye Kata zenu. Nawashauri muwakemee Watendaji wasiozingatia ubora katika usimamizi wa Miradi inayotekelezwa na pale inapobidi Mamlaka zishauriwe kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma.

iii. Zingatieni ratiba za vikao katika ngazi zote na hakikisheni Mikutano Mikuu ya Vijiji, Kamati za Maendeleo za Kata (WDCs) na Mabaraza ya Kata inafanyika. Iwapo Mikutano hiyo itafanyika kwa kuzingatia ratiba zake (na pale inapobidi kwa dharura) changamoto mbalimbali zinazowakabili Wananchi katika maeneo yenu zitapatiwa ufumbuzi.

iv. Simamieni na hakikisheni fedha kwa ajili ya Vikundi vya Wanawake,

Vijana na Walemavu zinatengwa na kutolewa kwa walengwa. Fedha hizi ni asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri (yasiyo ya masharti).

v. Fanyeni tathmini ya kina ya uwezo wa vyanzo vyenu vya mapato na wekeni mikakati inayotekelezeka ya kuongeza ukusanyaji wa mapato. Kwa mujibu wa taarifa zenu za mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri yenu ilikusanya mapato pungufu kwa asilimia **16** ya lengo la mwaka. Kutokana na hali hiyo, Halmashauri yenu ilikuwa na uwezo wa kujitegemea wa **asilimia 3** tu. *Hakikisheni mnatumia vyema Mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya Mapato.*

vi. Afisa Masuuli ahakikishe Wakuu wa Idara na Vitengo wote wanahusika katika utoaji wa taarifa muhimu kwa ajili ya kuandaa taarifa ya fedha. *Afisa Masuuli anapaswa kuhakikisha ubora na usahihi wa taarifa zinazowasilishwa kwa ukaguzi.*

vii. Afisa Masuuli aimarishe na kufuatilia kwa karibu utendaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (kwa kutoa fedha za kutosha, kukipangia Watumishi wa kutosha, kutoa mafunzo na vifaa/vitendea kazi) na kuimarisha Ufanisi wa Ukaguzi wa Ndani kama sehemu ya mfumo wa udhibiti wa ndani ya Halmashauri.

viii. Afisa Masuuli aimarishe Kamati ya Ukaguzi (ipewe fedha za kutosha, mafunzo na vitendea kazi) na ahakikishe inatimiza majukumu yake kikamilifu katika uangalizi wa mifumo ya utoaji taarifa za kifedha, taratibu

za kusimamia athari zinazotokana na shughuli za kifedha, udhibiti juu ya utekelezaji wa sheria, maadili, kanuni na taratibu.

ix. Fanyeni uhakiki wa ubora wa kitabu cha hesabu za mwisho kabla ya kuwasilisha kitabu husika kwa Mkaguzi.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri,

Kwa kuhitimisha;

- Natoa msisitizo kwamba Halmashauri iimarishe usimamizi wa vyanzo vya mapato na ufuatiliaji wa makusanyo ili kufikia lengo la makusanyo ya mwaka . *Kuweni wabunifu na ibueni vyanzo vipya vya mapato*.

- Zibeni mianya yote ya upotevu wa mapato. Halmashauri yenu inapoteza mapato mengi kutokana na udhaifu mkubwa wa baadhi ya Watendaji na mifumo ya ukusanyaji isiyosimamiwa vizuri.

- Endeleeni kutenga fedha za mapato ya ndani na kuzipeleka kuchangia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.

- Boresheni utoaji huduma na tatueni kero za Wananchi kwa wakati.

Akhsanteni kwa Kunisikiliza.